



**MAELEZO YA MHESHIMIWA MIZENGO PETER PINDA (MB)
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KWA WANANCHI KUHUSU SENA YA MAJARIBIO YA WATU
NA MAKAZI YA MWAKA 2011**

Ndugu wananchi,

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kufanya Sena ya Watu na Makazi hapo Agosti mwaka ujao.

MADHUMUNI YA SENA YA WATU NA MAKAZI 2012

Sena ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kama zilivyokuwa Sena zilizopita madhumuni yake makubwa ni kujua idadi ya watu na kukusanya taarifa za kina za kidemografia, kiuchumi, kijamii na maelezo ya makazi. Taarifa hizi hutumika na Serikali na Taasisi nyingine kwa shughuli mbali mbali za mipango na maendeleo. Serikali hutumia takwimu zitokanazo na Sena katika kutunga Sera, kufanya maamuzi juu ya Utawala wa Umma kwa kuzingatia mahitaji halisi na vigezo vingine kama vile vya umri, jinsi na vinginevyo.

Ndugu Wananchi,

Sena zote ni muhimu lakini Sena ya mwaka 2012 ina umuhimu wa kipekee kwa kuwa taarifa zitakazokusanywa zitatumika pia kutathmini Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umasikini Tanzania-MKUKUTA na Mkakati wa Kupunguza Umasikini Zanzibar-MKUZA. Takwimu hizo zitatumika pia kutathmini utekelezaji wa Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015.

SENSA YA MAJARIBIO

Ndugu wananchi,

Katika kuhakikisha kuwa Sena ya mwaka 2012 inafikia malengo na matarajio ya taifa Serikali imeandaa Sena ya

Majaribio. Sensa hii ya Majaribio ambayo, hufanyika mwaka mmoja kabla ya Sensa yenyewe, imepangwa ifanyike **JUMAPILI TAREHE 02 OKTOBA 2011** na inatarajiwa kumalizika ndani ya siku saba.

Lengo hasa la Sensa hii ya Majaribio ni kutathmini na kupima maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Kwa hiyo katika Sensa hii ya Majaribio tutapata usahihi wa nyaraka na kumbukumbu mbali mbali zitakazotumika zikiwemo madodoso (questinnaires), miongozo na fomu nyingine mbalimbali.

Halikadhalika Sensa hii ya Majaribio inalenga kupima ni kwa kiwango gani mfumo mzima wa Serikali yetu umejiandaa kufanya Sensa hiyo na kwa jinsi Wananchi kwa ujumla mtakavyoitikia wito wa kushiriki kwenye Sensa.

MAENEO YA SENA YA MAJARIBIO

Sensa ya Majaribio itazihusisha Kaya chache tu, zipatazo elfu tano (5000) zilizoko katika maeneo 44 ya kuhesabia watu kwenye Mikoa kumi na moja (11). Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Kaskazini Pemba, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mjini Magharibi, Mtwara, Njombe na Pwani.

Maeneo haya yamechaguliwa kwa kuzingatia uwakilishi wa jamii mbali mbali hapa Nchini na Viongozi wa maeneo husika wamejulishwa na wanaendelea na maandalizi yote muhimu.

WITO WANGU KWENU

Kwa hiyo wito wangu kwenu Ndugu Wananchi wakazi wa maeneo hayo yaliyochaguliwa kwa majaribio ni kuwaomba mshiriki kikamilifu katika Sensa hii kwa kushirikiana vyema na makarani wa Sensa (Enumerators) watakaofika katika maeneo yenu kwa kujibu maswali kwa ufasaha na kwa usahihi.

Napenda kuisisitiza kuwa majibu yenu ya maswali yaliyomo katika madodoso ya Sensa hii ya Majaribio yatatunzwa kwa siri kubwa na kuwa ndio yatakayotupa mwanga kama kweli madodoso yetu yanakidhi malengo ya Sensa yetu ya Watu na Makazi itakayofanyika mwaka 2012.

Namalizia kwa kuwatakia mafanikio mema katika kazi hii muhimu ya taifa.

SENSA KWA MAENDELEO: JIANDAE KUHESABIWA

Ahsanteni sana.

Mizengo P. Pinda
Mizengo P. Pinda (Mb)
WAZIRI MKUU